

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
MASUALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2017 HADI  
JANUARI, 2018**

Ofisi ya Bunge,  
S. L. P 941,  
**DODOMA**

Februari, 2018.

# YALIYOMO

<b><u>SEHEMU YA KWANZA</u></b> .....	<b>1</b>
<b><u>1.0 UTANGULIZI</u></b> .....	<b>1</b>
<u>1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati</u> .....	1
<u>1.2 Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati</u> .....	2
<u>1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati</u> .....	2
<b><u>SEHEMU YA PILI</u></b> .....	<b>3</b>
<b><u>2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI</u></b> .....	<b>3</b>
<u>2.1 Maelezo ya Jumla</u> .....	3
<u>2.2 Utekelezaji wa Shughuli za Kamati</u> .....	4
<u>2.3 Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati</u> .....	4
<u>2.4 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali..</u>	5
<u>2.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati</u> .....	11
<u>2.6 Uchambuzi wa Miswada</u> .....	30
<u>2.7 Ziara</u> .....	30
<u>2.8 Semina kwa Wajumbe wa Kamati</u> .....	31
<b><u>SEHEMU YA TATU</u></b> .....	<b>32</b>
<b><u>MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA</u></b> ....	<b>33</b>
<b><u>SEHEMU YA NNE</u></b> .....	<b>46</b>
<b><u>4.0 HITIMISHO</u></b> .....	<b>46</b>
<u>4.1 Shukrani</u> .....	46
<u>4.2 Hoja</u> .....	48

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2017 HADI JANUARI, 2018

---

## i. SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

### 1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni:

- (a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS);
- (b) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kanuni hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa Sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya. Kamati hii imepewa jukumu la:-

- a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;
- b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Madawa ya Kulevya;
- c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya; na
- d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

## **1.2 Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Kamati inateleleza Majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitumia utaratibu ufuatao:-

- (a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi kwa kuiomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa Taarifa juu ya jambo au suala mahsusi ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa Wizara na Taasisi hizo;
- (b) Kufanya ziara katika maeneo yenye maambukizi makubwa ya VVU na yenye mambukizo madogo;
- (c) Semina na kongamano mbalimbali zilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya; na
- (d) Kufanya mikutano na Wadau kwa lengo la kupokea maoni yao juu ya Masuala mbalimbali ambayo Kamati ilikuwa inafanyia kazi ikiwemo Muswada.

## **1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa na usimamizi

wa kutosha wa majukumu yake kwa mujibu kwa Kanuni za kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari 2017, Kamati ili kutekeleza shughuli zifuarazo:-

- ii. Kupokea mafunzo;
- iii. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara mbalimbali, Taasisi, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ;
- iv. Ziara
- v. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- vi. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- vii. Uchambuzi wa Muswada wa Sheria ; na
- viii. Kupokea Semina mbalimbali.

## **ix. SEHEMU YA PILI**

### **2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

#### **2.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, imefanya utekelezaji wa majukumu yake katika Mwaka 2017 kupitia mbinu mbalimbali,<sup>3</sup> kwa mujibu wa Kanuni za

Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kama ilivyoeelelezwa hapo awali. Aidha, majukumu hayo ni kama yalivyoeelekezwa ambayo pia Kamati itaeleza katika uchambuzi wa utekelezaji wake katika Taarifa hii.

## **2.2 Utekelezaji wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa;-

## **2.3 Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa Wabunge (Wajumbe) wa kamati hii walikuwa wapya ilikuwa ni muhimu kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu ya Kamati kuwapatia mafunzo Wajumbe ambayo yaliandaliwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Mafunzo haya yalifanyika kuanzia tarehe 10 hadi 11 Januari, 2017 Ofisi ya Bunge Dodoma. Mafunzo haya yalikuwa na faida na yaliwawezesha Wajumbe kufahamu muundo na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Elimu waliyoipata kupitia semina hizi iliwawezesha wajumbe kuelewa kwa undani taasisi watakazozisimamia na namna ambavyo wataweza kupambana na gonjwa la UKIMWI na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya.

## 2.4 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali

### (a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Tanzania (TACAIDS)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Tume hii ambayo ilionesha kuwa, takwimu za utafiti wa hali na viashiria vya UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2016/17 zinaonesha kuwa idadi ya raia wa Tanzania inakisiwa kuwa ni **50.9** milioni. Ukubwa wa maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kitaifa miongoni mwa jamii yenye umri wa miaka 15 – 49 ni wastani wa asilimia **4.7** kitaifa, wanawake wakiwa asilimia **6.2** na wanaume ni asilimia **3.1**. Inakadiriwa kuwa jumla ya watanzania **million 1.4** wanaishi na Virusi Vya UKIMWI. Na kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 15 na 24 ni asilimia **1.4**. Wavulana asilimia **0.6** na wasichana ni asilimia **2.1**.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti za awali zilizofanyika miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 15 – 49 zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya VVU yamekuwa yakipungua kutoka idadi ya watu **72,000** kwa mwaka 2013 hadi kufikia watu **48,000** kwa mwaka 2015. Hata hivyo, umri wa walengwa wa utafiti uliongezwa kutoka 15 – 64 katika tathmini ya mwaka 2016/17. Matokeo ya utafiti huo yamebainisha kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka 2016/17 yamefikia watu **81,000**.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la idadi hii kwa mwaka 2017 ni ishara mbaya kwetu jambo ambalo linahitaji uwajibikaji wa pamoja

kutoka ngazi ya mtu binafsi hadi ngazi ya kitaifa kwa kushirikiana kimkakati ili kufikia malengo ya kuzuiya maambukizi mapya ya VVU hatimaye kufikia sifuri (0)

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa baadhi ya mikoa ina maambukizi ya VVU sawa au zaidi ya kiwango cha Taifa cha asilimia **4.7**. Mikoa hiyo ni: Njombe asilimia **11.4** , Iringa asilimia **11.3**, Mbeya asilimia **9.3**, Mwanza **7.2**, Kagera **6.5**, Shinyanga **5.9** na Katavi **5.9**; Songwe **5.8**, Rukwa asilimia **6.2**, Dar Es Salaam asilimia **4.7**, Ruvuma asilimia **5.6** na Pwani **5.5**. Mikoa miwili yenye maambukizi kidogo ni Lindi **0.3** na Arusha **1.9** kwa Tanzania Bara. Maambukizi ni madogo zaidi kwa upande wa Tanzania Visiwani ambapo Unguja ni asilimia **1.2** na Kusini Pemba ni asilimia **0.3**.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kwamba karibu kila mtu wa umri baina ya miaka kumi na tano hadi miaka arobaini na tisa (15 - 49) amesikia kuhusu UKIMWI. Kwa bahati mbaya, wenye uelewa wa kina kuhusiana na maambukizi mapya ya VVU na njia za kujikinga bado ni chini ya nusu ya wale ambao wamesikia kuhusu UKIMWI. Aidha, kwa upande wa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 kiwango cha uelewa halisi kwa wasichana ni asilimia **40** ambapo kwa wavulana ni asilimia **47**. Hii inaonyesha kuwa vijana wetu wana uelewa mdogo wa Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI na hivyo kuwa katika hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya ya VVU.



**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya mwitikio kwa masuala ya VVU na UKIMWI nchini ambayo yamethibitishwa na takwimu, takwimu zinazoonyesha kuwa kiwango cha maambukizo mapya ya VVU kilishuka kwa zaidi ya 20% kati ya mwaka 2010 na 2015. Aidha, zaidi ya nusu ya WAVIU wanapata dawa ya kufubaza VVU (ARVs). Asilimia **86%** ya wanawake wajawazito wanaoishi na VVU wanapata dawa za kufubaza VVU (ARVs), hivyo dawa hizi zimesaidia kupunguza maambukizo mapya ya VVU kwa watoto (miaka 0 – 4) kwa takribani nusu (**50%**) kati ya mwaka 2010 na 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio haya, kumekuwepo na changamoto nyingi ambazo zitahitajika kufanyiwa maboresho ili kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika mwitikio kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI:-

- a) Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 imekuwa ya muda mrefu na mambo mengi yanayohusiana na masuala ya UKIMWI yamebadilika kwa maana hiyo, sera hii inahitaji kupitiwa upya ili kuiboresha.
- b) Maendeleo ya utafiti wa chanjo dhidi ya UKIMWI nchini bado ni kitendawili kwa maana hatujui tumefikia hatua gani kitaalamu.
- c) Ulinzi duni wa makundi ya watu kama wafungwa na watoto wanaoishi katika mazingira magumu ndiyo wako katika hatari zaidi;
- d) Msisitizo mdogo wa umuhimu wa kushiriki katika ngazi ya jamii na uwajibikaji kwa ajili ya utekelezaji wa mwitikio wa Taifa kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI;

e) Ukosefu wa mikakati endelevu ya kushughulikia uwezo wa kaya kuboresha desturi za kulisha watoto lishe bora na huduma za lishe bora kwa WAVIU;

## **LISHE NA UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) na wanaotumia dawa wanakabiliwa na lishe duni hususani kwa watoto wanaoishi na virusi. Kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha program ya lishe ikiwa ni pamoja kuhamasisha viwanda kuweka virutubishi kwenye unga na mafuta ya kupikia. Kamati inashauri elimu zaidi bado inahitajika kuhusu lishe bora iendeleo kutolewa katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha viwanda vidogo vidogo kuongeza virutubishi.

## **UKATILI WA KIJINSIA**

**Mheshimiwa Spika**, tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa, ukatili wa kijinsia (Gender Based Violence) ni chanzo cha maambukizi mapya ya VVU. Ukatili wa kijinsia unajumuisha unyanyasaji wa kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Hata hivyo kuna baadhi ya mila zimekuwa hatarishi kwa kuchangia maambukizo mpya ya VVU zikiwemo ndoa za utotoni, kurithi wajane bila ya kujua afya ya anaerithiwa wala anaerithi na ngono zembe.

## **UKEKETAJI**

**Mheshimiwa Spika**, suala la ukeketaji (Genital Mutilation) mbali na kuwa miongoni mwa masuala ya unyanyasaji wa Kijinsia, desturi

zinazosababisha mwanamke kunyimwa haki yake kimsingi ya kibinaadamu, pamoja na kupata maambukizi mapya ya VVU kwa utumiaji wa vifaa visivyo salama. Aidha, imedhihirika kuwa kiafya ni kitendo ambacho humweka mwanamke katika hatari kubwa ya kutokwa na damu nyingi na hatimaye kupoteza maisha hususan wakati wa uzazi. Hivyo, hatuna budi kuhakikisha tunaunganisha nguvu zetu ili kuondokana na tatizo hili.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inatoa wito kwa wananchi kuzingatia maudhui ya kampeni mbalimbali zinazofanywa na Serikali na wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadili tabia, kuachana na mila hatarishi na kujikinga na maambukizo mapya ya VVU.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Jeshi la polisi kuanzisha dawati la jinsia kwenye vituo vyote vya polisi ambapo kazi yake kubwa ni kusikiliza malalamiko na kupokea taarifa kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia bado kumekuwepo na kukithiri kwa vitendo vya ukatili.

**Mheshimiwa Spika** ili kupunguza maambukizi ya VVU na ukatili wa kijinsia, Kamati inaishauri serikali kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya mambo ya ndani ya nchi kuliangalia suala hili ili kupata mikakati thabiti ya kupunguza ukatili wa huo ambao unachangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya UKIMWI.

## **MFUKO WA UDHAMINI WA KUDHIBITI UKIMWI (AIDS TRUST FUND – ATF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Mfuko huu ambapo ilionesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya gharama za UKIMWI kwa mwaka zinafadhiliwa na wadau wa maendeleo wa Serikali ya Marekani na Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

**Mheshimiwa Spika,** ili kupunguza utegemezi huo kutoka kwa wafadhili, Mfuko ulijiwekea malengo ambayo ni kuongeza rasilimali fedha za ndani kutoka asilimia **7** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **30** ifikapo mwaka 2018, pamoja na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika udhibiti wa UKIMWI kutoka asilimia 8 hadi asilimia 15 kufikia 2018. Madhumuni ya Mfuko huu ni pamoja na:-

- a) Kuhakikisha kunakuwepo na vyanzo endelevu kwa ajili ya mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI Tanzania Bara.
- b) Kupunguza utegemezi katika kugharimia shughuli za mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.
- c) Nchi kuweza kufanya maamuzi yake yenyewe katika utekelezaji wa afua za UKIMWI.

Aidha, maeneo yaliyoanishwa kushughulikiwa na mfuko huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Asilimia 60 ya pesa za mfuko zitatumika kwa ajili ya

upatikanaji wa vifaa tiba na dawa kama vile ARVs na condoms kwa ajili ya watu wazima, wanawake, wajawazito, watoto na vijana waliofikia umri wa kubalee .

(ii) Asilimia 25 zitatumika kwa ajili ya kinga: ushauri nasihi na kupima, elimu ya uzazi na program zinazolenga kubadili tabia.

(iii) Asilimia 15 zitatumika kwa ajili ya mazingira wezeshi ikiwa ni tathimini ya ufuatiliaji, utafutaji wa rasilimali (resource mobilization) na madhara yatokanayo na UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo na vipaumbele vilivyowekwa katika kutimiza majukumu ya Mfuko huo, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali, moja wapo ikiwa ni kukosekana kwa chanzo cha uhakika na endelevu cha fedha za Mfuko ambacho kingesaidia kupatikana fedha na kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili kutoka nje ya nchi kwani kwa sasa nchi inategemea ufadhili wa afua za UKIMWI kwa asilimia 90.

## **2.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati**

### **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia ufanisi wa utekelezaji wa Mwongozo wa utumiaji na ugawaji wa Fedha za UKIMWI kwenye Halmashauri na Manispaa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, OR- TAMISEMI huangalia maeneo yenye mapungufu (gaps) hivyo kuweka vigezo vitakavyotumika katika kuihudumia Mikoa na Halmshauri katika program za ugawaji wa fedha za UKIMWI ambapo, ni pamoja na kuangalia hali ya maambukizi makubwa ya UKIMWI kutokana na tafiti zilizofanyika, kwa hiyo basi kipaumbele hutolewa kwenye maeneo yenye ukosefu au upungufu wa huduma za VVU na UKIMWI na kutokuwepo au kuwepo kwa wadau/ Asasi wachache wanaofanya shughuli za kuhudumia jamii katika mapmbano dhidi ya UKIMWI/VVU.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi juni, 2017 jumla shilingi bilioni **2.63** zilitolewa kwenye Mikoa na halmashauri. Aidha, Mikoa ilipata shilingi bilioni **2.31** sawa na asilimia **78.8** na halmashauri shilingi milioni **320** sawa na asilimia **21**. Aidha, Mikoa ilipata fedha nyingi kwa ajili ya kuendeshea mafunzo kwa watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kutoa huduma stahiki kulingana na miongozo. Fedha zilizotolewa kwenye Halmashauri ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma katika vituo vya afya katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilielezwa changamoto za kuongezeka kwa idadi kubwa ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, watu wanaoishi na VVU ukilinganisha

na kiwango cha fedha kilichokuwa kinapatikana, uelewa mdogo kwa baadhi ya watu wanaoshi na VVU , kutozingatia matumizi sahihi ya dawa za kupunguza makali ya VVU pamoja na unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU. Hii husababisha watu kutojitokeza kupima VVU au kutosubiri majibu ya vipimo au kwenda mbali katika kituo cha kutolea huduma mahali ambapo hawafahamiki.

(i) **WIZARA YA MAMBO YA NDANI (JESHI LA MAGEREZA)**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilipata fulsa ya kukutana na Wizara ya Mambo ya Ndani (Jeshi la Magereza) ili kupokea Taarifa kuhusu hali ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Magerezani pamoja na upatikanaji wa kinga na tiba ya magonjwa nyemelezi. Katika mahojiano hayo Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Magereza lina jukumu la kuhakikisha kwamba, wafungwa na mahabusu wanapata huduma bora za afya kama ilivyo kwenye jamii nyingine ikiwa ni pamoja na kumwona daktari, uchunguzi wa afya, tiba, ushauri nasaha na upimaji wa VVU.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa, Jeshi la Magereza kwa mwaka 2015/2016 walipima jumla ya wafungwa na mahabusu **8,287**; kati yao waliokutwa na maambukizi ya UKIMWI walikuwa **376**, sawa na asilimia **4.5%**. Aidha, kwa mwaka 2016/2017 Jeshi la Magereza lilipima jumla ya wafungwa/mahabusu **34,793** (wanawake **1,451** na wanaume **33,342**) kati yao waliokutwa na

maambukizi ni **953** (wanaume 818 na wanawake 135) sawa na asilimia **2.7**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa uwepo wa msongamano mkubwa wa wafungwa/mahabusu unaoathiri utoaji wa huduma bora kwa wafungwa na kwamba, hivi sasa kuna wafungwa na mahabusu **39,312** wakati uwezo wa magereza ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu **29,552**. Aidha, pamoja na msongamano mkubwa kuna ufinyu wa bajeti ambao umesababisha Miradi ya Afya kutotekelezwa, upungufu wa dawa, vifaa, vifaa tiba na chakula lishe kwa wafungwa, mahabusu na watumishi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- (a) Ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu/magerezani, Serikali itumie adhabu mbadala kwa makosa madogo madogo. Kwa kufanya hivyo, kutapunguza msongamano, gharama kwa Serikali na uwezekano wa kuambukizana magonjwa kama vile Homa ya Ini, UKIMWI na Kifua Kuuu.
- (b) Jeshi la Magereza liongezewe bajeti kwa ajili ya chakula pia libuni mkakati wa kuwatumia wafungwa hususan wanaotumikia vifungo vya muda mrefu kuongeza uzalishaji ili kujitosheleza kwa chakula pamoja na kuongeza maduhuli ya Serikali. Aidha, serikali itoe motisha kwa wataalam wa afya walioko Magereani ili waendeleo kubaki na kutoa huduma stahili kwa wafungwa na mahabusu.



(c) Elimu ya mara kwa mara itolewe kwa wafungwa na mahabusu ili wapate uelewa wa namna ya kupambana na janga la UKIMWI. Aidha, Kamati inashauri wafungwa wote wapatiwe chanjo ya kuzuia ugonjwa wa homa hatari ya Ini.

(d) Shughuli zozote zinazohusu madawa ya kulevya na UKIMWI Magerezani, Uongozi wa Magereza uwahusishe Waratibu wa UKIMWI na dawa za kulevya wa Mikoa na Wilaya husika ili kubadilishana uzoefu na elimu.

### (ii) **BOHARI KUU YA DAWA NCHINI (MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utendaji wa MSD ilionesha kuwa dawa za UKIMWI hununuliwa na kupokelewa kutoka nje ya nchi. Manunuzi ya dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs) yamegawanyika katika makundi mawili ambayo kundi la kwanza ni dawa za ARVs ambazo hununuliwa na wafadhili wa Global Fund moja kwa moja kwa mfumo wa ((Pooled Procurement Mechanism), ambapo dawa hutolewa nchini na washitiri kulingana na mahitaji na maoteo ya Mpango wa Kudhibiti UKIMWI (NACP). Kundi la pili ni vitendanishi vya maabara (Laboratory Reagents) ambazo hununuliwa na MSD kulingana na mahitaji yanayoletwa na kitengo cha Taifa cha Kudhibiti UKIMWI- National AIDS Control Programme ( NACP)

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilijulishwa kuwa hali ya upatikaji wa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI (ARVs) pamoja na vitendanishi zinapatikana kwa asilimia 100 na MSD ina dawa

ghalani zenye uwezo wa kutosha kwa matumizi ya wastani miezi 6 hadi 15. Kamati inaipongeza serikali kwa juhudi wanazofanya za kuhakikisha kuwa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vinapatikana kwa wakati katika hospitali zote nchini bila upungufu wa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, idadi ya watoto wanaozaliwa na akina mama walio na maambukizi ya VVU/UKIMWI inaendelea kupungua siku hadi siku kutokana na akina mama hao kujiunga na mpango wa kutokomeza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto Elimination of Mother to Child Transmission (eMTCT). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa maambukizi ya VVU/UKIMWI yamepungua. Hata hivyo, Serikali iongeze juhudi katika usambazaji wa mashine ya viral load katika hospitali zote za mikoa na wilaya hasa ukizingatia kwamba kwa sasa mashine hizo zipo chache ukilinganisha na mahitaji. Aidha, Kamati inashauri pia dawa aina ya **Septine** inayotibu magonjwa nyemelezi iongezwe kwenye orodha ya dawa za ARVs ambazo hutolewa bure kwa WAVIU. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa shilingi Milioni **600** kwa ajili ya kununua dawa aina ya **Septine**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana kutokana na upatikanaji wa dawa na vitendanishi. Kamati ilielezwa chagamoto mbalimbali kama ifuatavyo;

(i) Upungufu na upatikanaji wa dawa za kuzuia magonjwa

- nyemelezi kutokana na ufinyu wa bajeti ya serikali baada ya wafadhili kujitoa kununua dawa hizo;
- (ii) Dawa na vitendanishi zinanunuliwa kwa pesa ya wafadhili ambapo bajeti yake ni zaidi ya shilingi bilioni 200;
  - (iii) Mabadiliko katika matumizi ya dawa za ARVs (treatment regimen) hupelekea kubadilishwa kwa matumizi yake na hivyo kupelekea kuchina kwa dawa na vitendanishi;
  - (iv) Bohari kuu ya dawa nchini kutoruhusiwa kununua dawa za ARVs kwa fedha za Mfuko wa Dunia (Global Fund) na hivyo kutegemea fedha za mgao wa kawaida wa dawa. na;
  - (v) Bidhaa zote za UKIMWI hupatikana nje ya nchi na hivyo kuongezeka kwa gharama za utunzaji na upatikanaji.

#### **(iv) KITENGO CHA KUDHIBITI UKIMWI NCHINI (NACP).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI ambapo ilionesha kuwa viwango vya mambukizi ya virusi vya UKIMWI miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 15 – 49 vimeshuka kutoka asilimia **7** mwaka 2003/2004 na kufikia asilimia **5.7** mwaka 2007/2008 na kuendelea kushuka kutoka asilimia **5.7** hadi asilimia **5.1** mwaka 2011/2012. Kwa mujibu wa takwimu za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI idadi ya watu waliopatiwa huduma za ushauri na kupima VVU kwa kwa hiari imeongezeka hadi kufikia watu **42,021,146** mwezi Juni 2017 pamoja na kuongezeka kwa vituo vya ushauri nasaha na kupima VVU kwa hiari kutoka vituo **59** mwaka 1997 hadi kufikia vituo **6259** mwezi

Machi, 2017. Idadi hii inajumuisha vituo vyote vya serikali na visivyo vya serikali.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia Juni 2017 watu wanaoishi na VVU na UKIMWI wapatao **951,595** sawa na asilimia **2.3** walipatiwa huduma za tiba na mafunzo. Kati yao walioanzishiwa dawa watoto na watu wazima ni **935,228**. Sawa na asilimia **2.2** miongoni mwao ni watoto chini ya miaka 15 ni **59,704**, vijana waliobalehe wenye umri kati ya miaka 15 -19 ni **20,845**. (Taarifa ya kitengo cha Taifa cha Kudhibiti UKIMWI- National AIDS Control Programme - NACP, Juni 2017).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza serikali kwa juhudi wanazofanya kwani unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU umepungua, utafiti wa viashiria vya UKIMWI na Malaria nchini wa mwaka 2011/2012 unaonyesha kwamba wanawake na wanaume zaidi ya asilimia **90** wako tayari kumhudumia mwanafamilia mwenye UKIMWI katika familia zao. Aidha, katika kuimarisha afya za wananchi wanaoishi na VVU kwa mwaka 2016/2017 mashine kubwa na za kisasa zenye uwezo wa kupima wingi wa VVU (HIV Viral Load Monitoring) kwa sampuli (192 kwa mkupuo) zimefungwa katika hospitali ya Taifa Muhimbili, hospitali ya Temeke, hospitali ya rufaa Mbeya, na hospitali za mikoa ya Iringa, Ruvuma, Lugalo, Bugando, Tabora, Mtwara, Morogoro, Arusha, Dodoma, Rukwa, na Rubya Mkoani Kagera.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa pia kuhusu changamoto ya ufinyu wa rasilimali watu na fedha za kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI pamoja na baadhi ya watu wanaotumia dawa za ARVs kushindwa kuzingatia matumizi sahihi na endelevu ya ARVs. Pia, ushiriki mdogo wa wanaume na wenza katika kutumia huduma za VVU na UKIMWI.

(b) **Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inalo jukumu la kufuatilia utekelezaji wa serikali kuhusu Sera na Mipango ya udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati iliweza kukutana na Mamlaka hiyo ili kupokea na kujadili taarifa juu ya masuala ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imekuwa ikifanya kazi ya kubaini na kuharibu mashamba ya bangi, kuzuia uvunaji wa mirungi, kupeleleza na kuchunguza uchepushaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevya pamoja na kemikali zilizosajiliwa kutoka kwenye vyanzo halali. Wakati huo huo kuhakikisha dawa hizo zinapatikana kwa matumizi ya tiba, biashara na mahitaji ya kisayansi pamoja na kuzuia biashara haramu ya dawa za kulevya na kuteketeza dawa zilizokamatwa na kuzuia utengenezaji haramu wa dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na serikali katika kupambana na dawa za kulevya kwani kasi ya

ukamataji wa dawa za kulevya imeongezeka, kuteketezwa kwa kiasi kikubwa cha mshamba ya bangi na kutambua na kudhibiti njia mbalimbali za kupitisha na kusafirisha dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Mamlaka pamoja na wadau wengine katika kufanikisha uanzishwaji kwa huduma ya tiba za utengemao wa warahibu katika mkoa wa Mbeya. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa juhudi za haraka zifanyike ili mikoa ya Mwanza na Dodoma ianze kutoa huduma hiyo kwa kuwa majengo kwa ajili ya kutumika ili kutoa huduma hiyo yapo. Pamoja na jitihada hizo, kuna haja ya Serikali kuendelea kuihuisha huduma hii katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika katika Masuala ya UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima. Aidha, dirisha la kutolea huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya lianzishwe katika hospitali zote za rufaa na za mikoa yote nchin ili kuweza kuwafikia waathirika wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kuwa huduma hii inakuwa endelevu. Vile vile Kamati inaishauri serikali kuanzisha huduma hii katika hospitali zote nchini pamoja na kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo na stadi mbalimbali pamoja na mitaji itakayowawezesha waathirika wa dawa za kulevya kuweza kujikimu kimaisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokutana na Mamlaka ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya iliweza kubaini changamoto zifuatazo:-

- (i) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haina bajeti ya kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ukamilifu mfano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mamlaka imetengewa kiasi cha shilingi **3.4** Bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hii haitoshelezi kutokana na ukweli kwamba inahitaji kufanya operesheni nyingi za kudhibiti ulimaji na usafirishaji wa dawa za kulevya kama bangi na mirungi nchi nzima. Pia Mamlaka inahitaji kufungua ofisi za kanda ili kupanua na kusogeza huduma yake mikoani , kwani kwa sasa inafanya kazi kutokea makao makuu tu;
- (ii) Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo ya milimani ambako hakufikiki kwa urahisi hivyo kufanya operesheni za ukamataji kuwa na changamoto nyingi;
- (iii) Kukosekana kwa vitendea kazi vya kisasa vinavyosababisha kupungua kwa ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevya nchini;
- (iv) Mamlaka inashindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya Taifa kutokana na ufinyu wa bajeti;
- (v) Upatikanaji wa tiba za utengemao wa warahibu

wa dawa za kulevya nchini haujitoshelezi. Kwa sasa huduma hizi zinapatikana katika mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee; na

- (vi) Kukosekana kwa programu maalum zenye lengo la kuwainua kiuchumi warahibu wa dawa za kulevya ambao huchangia kukwamisha juhudi zao katika kuachana moja kwa moja na matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura ya 95) wa Mwaka 2017 (The Drug Control and Enforcement Amendment) Act, 2017. Hivyo kuifanya Mamlaka Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kuwa na nguvu na uwezo mkubwa wa kukamata, kuzuia na kupeleleza makosa mengine yanayojitokeza wakati wa kushughulikiaji/uchunguzi wa makosa mengine yatokanayo na dawa za kulevya. Aidha, kutokana na mabadiliko ya sheria hiyo Mamlaka sasa ina uwezo wa kumiliki na kutumia silaha pamoja na kuboresha na kupanua wigo wa taratibu za ukusanyaji ushahidi kwa kutumia vifaa vya kisasa na kieletroniki.

**(b) Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni ya mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na mchakato wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya



Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, mnamo mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa **Bajeti** imekuwa ni changamoto kubwa kwa kuwa Taasisi zote zimekuwa hazipewi fedha zilivyoidhinishwa na Bunge kama inavyoelezwa hapa chini:-

(a) **Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, mpaka Kamati inapokea Taarifa mwezi Machi, 2017, hata nusu ya Bajeti ilikuwa haijatolewa, kwa mfano, katika mwaka wa Fedha 2016/2017, kati ya shilingi **bilioni 10.1** zilizokuwa zimetengwa ni shilingi **2.7 bilioni** sawa na asilimia **27** ya bajeti ndizo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini changamoto hiyo, Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kutoa maoni yake ambayo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 6<sub>23</sub> April, 2017.

## **Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)**


**Mheshimiwa Spika**, katika kikao chake kilichofanyika tarehe 25 Machi, 2017, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadilio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo inaonesha kuwa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kutoka *shilingi* **10,192,509,413/=** hadi shilingi **5,983,975,859** sawa asilimia **50**, pamoja na serikali kuanzisha Mpango wa Test and Treat kwa ajili ya kutoa dawa pale mtu atakapopatikana na maambukizi ya VVU kuanza kutumia dawa za kufubaza maambukizi ya UKIMWI bado bajeti hii imepungua. Kamati ilibaini changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo kwa kiasi kikubwa zilisababishwa na ufinyu wa bajeti zilizotengwa na Serikali kwa Tume hii kama zinavyoonyeshwa katika majedwali na chati ifuatayo:

### **JEDWALI NAMBA 1**

#### **MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE MFULULIZO KUANZIA 2013/2014 HADI 2017/2018**

<b>MWAKA</b>	<b>FEDHA ZA MAENDELE O</b>	<b>MATUMIZI YA KAWAIDA</b>	<b>JUMLA</b>	<b>MAONI</b>
2017/2018	3,455,342,560	2,528,633,299	5,983,975,859	

MWAKA	FEDHA ZA MAENDELE O	MATUMIZI YA KAWAIDA	JUMLA	MAONI
2017/2018	3,455,342,560	2,528,633,299	5,983,975,859	
2016/2017	5,235,823,413	4,961,677,000	10,197,500,413	Bajeti inajumlisha Fedha za Mfuko wa UKIMWI Bilioni 5.6
2015/2016	2,744,438,000	6,387,068,000	9,131,506,000	Bajeti inajumlisha Fedha za Mfuko wa UKIMWI
2014/2015	5,341,286,000	3,358,663,400	8,699,949,400	
2013/2014	5,341,286,000	3,082,866,000	8,424,152,000	



**Chanzo: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa miaka ya fedha 2013/2014, 2014/15, 2015/16, 2016/17 na 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilikuwa inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **25,000,000/=**. Aidha, Bajeti ya Tume ilianza kupungua katika kipindi cha mwaka 2013/2014 na kuwa katika hali yakupanda na kushuka hadi mwaka 2015/2016 kutokana na kupungua kwa mtiririko wa fedha za wafadhili katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha, kupanda na kushuka kwa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2017/2018, kumesababishwa na ukomo wa bajeti ya Serikali. Kwa kiasi kikubwa mwenendo huu wa bajeti umeathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI nchini.

(b) **Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**  
**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ilikuwa ya kuridhisha. Utendaji wa Taasisi hii ulikuwa wa Kuridhisha kutokana na mwenendo wa utoaji wa fedha kwani katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za

Kulevya ilitengewa kiasi cha shilingi **2.3 bilioni**, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kiasi kilichopokelewa ni shilingi **milioni 851**. ambayo ni sawa na asilimia **37** ya fedha iliyotengwa. Kamati inaridhishwa na mwenendo huu wa utoaji wa fedha kwani ikumbukwe kuwa dawa za kulevya ni kama Janga la Taifa linaloathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha utasaidia kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya dawa hizo, hivyo na kuendelea kuwabaini na kuwakamata watuhumiwa na kuokoa vizazi vyetu na kuwa na Taifa lenye afya njema.


**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 26 Machi, 2017 Mkoani Dodoma, pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:

#### **JEDWALI NAMBA 2:**

**MWENENDO WA BAJETI YA ILIYOKUWA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NA BAADA YA KUUNDWA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO**

**MFULULULIZO KUENZIA 2013/2014 HADI 2017/2018**

<b>MWAKA</b>	<b>FEDHA ZA MAENDELEO</b>	<b>MATUMIZI YA KAWAIDA</b>	<b>JUMLA</b>	<b>MAONI</b>
2017/2018	0	4,015,912,9 91	4,015,912,9 91	
2016/2017	0	2,340,236,0 00	2,340,236,0 00	
2015/2016	860,000,000	2,159,488,3 59	3,019,488,3 59	
2014/2015	3,430,000,0 00	3,601,549,7 18	7,031,549,7 18	Bajeti inajumlisha Fedha za Wafadhili
2013/2014	2,798,000,0 00	2,587,176,8 26	5,385,176,8 26	Bajeti inajumlisha Fedha za Wafadhili



**Chanzo:** Bajeti za Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya kwa miaka ya fedha 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17.

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kipindi cha mwaka 2013/2014 ilikuwa chini ikilinganishwa na 2014/2015, ambapo kushamiri kwa biashara ya dawa za kulevya uliongezeka na bajeti ya Tume hiyo iliongezeka kutokana na umakini wa Serikali na wafadhili katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017, bajeti za Tume zilishuka hadi kufikia shilingi **0** kwa miradi ya maendeleo ambako kulisababishwa na mabadiliko ya vipaumbele vya wafadhili husika katika mwaka 2016/2017. Kwa mwaka 2017/2018 Bajeti ya Mamlaka imeongezeka kwa shilingi **1,675,676,991/=** na kufikia Shilingi **4,015,912,991/=** ikilinganishwa na shilingi **2,340,236,000** zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **72** na hivyo kuchangia katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa

Mamlaka katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

## 2.6 Uchambuzi wa Miswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Novemba, 2017, Kamati ilijadili na kuchambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura ya 95) wa Mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement (Amendment) Act, 2017*). Marekebisho ya Muswada huu yaliwasilishwa Bungeni na kupitishwa kuwa Sheria.

## 2.7 Ziara

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Njombe na Iringa. Kutokana na ziara hizo, Kamati imebaini bado upo ukatili kwa wanawake na watoto unaosababishwa na mila na desturi pamoja na mfumo dume uliotawala katika jamii hizo, ambao unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya VVU licha ya jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na janga hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada katika kukomesha mila na desturi potofu zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU hata ikibidi kutumia vyombo vya dola. Aidha, Kamati inaupongeza Mkoa wa Manyara na



Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha maambukizi yanashushwa na kuwa kiwango cha chini kitaifa.

## 2.8 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipewa semina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe. Semina hizo ni pamoja na:

### (a) Semina ya Uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI walipatiwa mafunzo kwa njia ya semina iliyoendeshwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (*UNDP*) chini ya Mradi unaojulikana kama *Legislative Support Program (LSP II)* iliyo chini ya Ofisi ya Bunge. **Katika semina hiyo wajumbe walijengewa uwezo wa namna ya kuchambua Bajeti ya Serikali hususan upangaji wa vipaumbele vya Taifa.** Semina hiyo iliyofanyika tarehe 25 Oktoba, 2017 katika Ukumbi wa African Dreams Dodoma.

### (b) Semina ya Hali ya UKIMWI Tanzania

Semina hii iliendeshwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*). Semina ilieleza kuwa kiwango cha uambukizo kinashuka katika jamii pamoja na idadi ya maambukizi mapya yanapungua kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2013 ambapo maambukizi mapya yalikuwa **72,000**, mwaka 2014 maambukizi mpya **69,603** na mwaka 2015 maambukizi mapya yalikuwa **48,000**. **Semina hii iliwawezesha Wajumbe kuelewa**

**umuhimu wa kuongeza mwitikio dhidi ya UKIMWI na kuongeza utashi wa kisiasa katika ngazi za jamii na Taifa ili kupambana na kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi mpya.** Semina hii ilifanyika tarehe 26 Novemba, 2017 katika Ukumbi wa Zahanati ya zamani Ofisi ya Bunge Dodoma.

**(c) Semina ya Sera, Sheria na Mikakati ya Afya**

Semina hii iliendeshwa na Shirika lisilo la Kiserikali la **Tanzania Council for Social Development (TACOSODE)**. Lengo lake lilikuwa ni pamoja na Shirika kujitambulisha kwa Wajumbe wa Kamati ili kuwaelezea kazi zinazofanywa na Shirika hilo, pia kuwapa uchambuzi kuhusu Sera, Sheria na Mikakati ya afya ya Tanzania na uhusiano wake na afua za VVU na UKIMWI miongoni mwa makundi maalum. **Semina ilisaidia kupanua uelewa wa Wajumbe wa Kamati kuhusu masuala ya UKIMWI katika makundi maalum ambayo ni makundi ya watu ambao wapo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa sababu ya tabia mbalimbali zinazofanywa na makundi hayo.** Semina hii ilifanyika tarehe 25 November, 2017 katika Ukumbi wa Zahanati ya zamani Ofisi ya Bunge Dodoma.

**x. SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa Maoni na Mpendekezo kama ifuatavyo:-

**xi. MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza vyema majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo manane (8) yafuatayo:-

1. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba ufinyu wa Bajeti ya Serikali kwa Mamlaka unasababisha kutotekeleza majukumu yake kwa ukamilifu, kwani kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **hakukuwa na fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.

**Mheshimwa Spika**, Fedha hii haitoshelezi na hivyo kukwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Mamlaka kama vile:-

- a) Kufanya operesheni nyingi za kudhibiti kilimo na usafirishaji wa dawa za kulevya kama bangi na mirungi nchi nzima pamoja na kudhibiti uingizwaji na usambazaji wa dawa nyingine za viwandani kama cocaine na heroin.
- b) Mamlaka inahitaji kufungua Ofisi za Kanda ili kupanua na kusogeza huduma zake mikoani kwa kuwa mpaka sasa Mamlaka inafanya kazi kutoka Makao Makuu tu.
- c) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa gumu;
- d) Mamlaka kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa<sub>33</sub> sehemu zisizofikika

kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo huhitaji fedha nyingi.

- e) Mamlaka kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya taifa letu ; na
- f) Kushindwa kufuatilia udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya ambapo wafanyabiashara wa dawa hizo wamebuni mbinu mpya ya kutumia kemikali na dawa nyingine za matumizi ya binadamu kutengeneza dawa za kulevya pamoja na kuibuka kwa maabara bubu zinazotumika kutengeneza dawa hizo hatari .

**Na kwa kuwa,** kutotekelezwa kwa majukumu ya msingi ya Mamlaka hiyo

kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudi za udhibiti wa dawa za kulevya nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa taifa;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa kipekee wa majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kufanikisha mapambano na kuiongezea ufanisi Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na hivyo kwa pamoja tunaweza kujenga jamii imara ya Watanzania kwa kuachana kabisa na matumizi, na biashara ya dawa hizo.

2. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kuwa, hakuna Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevya japo tayari kuna Sheria ya Udhhibiti wa Dawa za Kulevya;

**Na kwa kuwa**, Sera hii ni muhimu sana kwa taifa kwani hutoa dira ya jambo linalohusika na jinsi ya kulidhibiti;

**Na kwa kuwa** tayari Kamati imedokezwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwamba, mchakato wa utungaji wa sera hiyo umekwishanza kwa kukusanya maoni kwa wadau wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa Sera hiyo ili kulinusuru taifa na janga hili la dawa za kulevya.

3. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kutokuwepo kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri kama ilivyo kwa Kamati za UKIMWI kwa ngazi ya Halmashauri;

**Na kwa kuwa**, kukosekana kwa chombo hicho kama ilivyo kwa Masuala ya UKIMWI kunachangia udhibiti hafifu wa dawa za kulevya katika halmashauri nchini;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri.

4. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto za upatikanaji usiotosheleza wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya (*Medically Assisted Therapy*) nchini;

**Na kwa kuwa**, huduma hizo zinapatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam Mbeya na Zanzibar pekee, jambo ambalo linasababisha jamii kubwa ya Watanzania kutofikiwa na huduma hii;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali ifanye juhudi za haraka ili Mikoa ya Mwanza na Dodoma ianze kutoa huduma kwa kuwa majengo kwa ajili ya kutumika kutoa huduma hiyo yapo tayari.

(b) Serikali iendeele na kuihuisha huduma hii katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika katika Masuala ya UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

5. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevya punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo kama kutengwa na jamii na kukosa ajira;

**Na kwa kuwa**, hali hiyo huwapelekea kurudia tena matumizi ya dawa za kulevya au kujiingiza katika vitendo vya uhalifu na kuenea kwa magonjwa kama vile kifua kikuu na UKIMWI pamoja na usugu wa Tiba kwa magonjwa hayo unaochangiwa na matumizi ya dawa za kulevya;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha programu maalum za kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemea kiuchumi mara tu

baada ya kuachana na matumizi ya dawa hizo.

6. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kuwepo kwa mwamko mdogo na ushiriki hafifu wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya;

**Na kwa kuwa**, hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili, homa ya ini na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri:-

- a) Mamlaka ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali na kuwajengea uelewa Watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia itawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya;
- b) Viongozi Wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili; na
- c) Mafunzo kuhusu athari ya matumizi ya dawa za kulevya yaingizwe kwenye mtaala wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu haraka iwezekanavyo ili kuwapatia uelewa na hivyo kuinusuru Jamii ya Watanzania kutokana na athari hizo.

7. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba nyumba za upataji nafuu (*Sobber Houses*) zinamilikiwa na watu binafsi;

**Na Kwa kuwa**, nyumba hizo hazina miongozo ya namna ya kuwapokea na kuwahudumia waathirika wa madawa hayo japokuwa Kamati ilifahamishwa kwamba serikali imekwishaandaa rasimu ya mwongozo huo;

**Na kwa kuwa**, nyumba hizo kwa hivi sasa zinaendeshwa kibiashara kwa familia kuchangia kiasi cha Sh. 100,000 mpaka 200,000;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kwamba, Serikali ianzishe nyumba zake za kuwasaidia waarhika wa dawa za kulevya (*Sobber Houses*) kila Mkoa ili kuwahudumia Watanzania walioathirika na dawa hizo.

8. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba asilimia 100 ya dawa aina ya Methadone ambayo hutumika kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya nchini hutolewa na nchi muhisani kupitia kituo chake cha kudhibiti magonjwa ya kuambukiza (*Centre for Disease Control and Prevention - CDC*);

**Na kwa kuwa**, kufanya hivyo ni kuandaa bomu kwa siku za usoni kwa maana ufadhili huo unaweza kukoma muda wowote kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kuathiri maisha ya Watanzania;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa Bajeti kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo



ukizingatia kwamba mahitaji ni mengi na wanaofikiwa na huduma ya dawa hizo ni wachache.

## **TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (TACAIDS):**

**Mheshimiwa Spika**, ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo kumi (11) yafuatayo:-

1. **Kwa kuwa**, Sera ya UKIMWI ya Tanzania ya Mwaka 2001 imepitwa na wakati;

**Na kwa kuwa**, yapo mambo mengi yanayohusiana na masuala ya UKIMWI yamebadilika;

**Na kwa kuwa**, bado sera yetu haijaakisi masuala hayo;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wamapitio ya Sera ya UKIMWI ya Mwaka 2001 ili iweze kuzingatia mabadiliko katika mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI kitaifa na kimataifa.

2. **Kwa kuwa**, mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI yanategemea wafadhili kutoka nje ya nchi kwa asilimia 90;

**Na kwa kuwa**, Serikali imeanzisha Mpango wa **Test and Treat** ambapo mtu anapopatikana na maambukizi ya VVU humlazimu kuanza kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU mara moja, hivyo huongeza mahitaji na gharama za manunuzi ya ARVs;

**Na kwa kuwa**, katika nchi yetu wafadhili walio wengi

wamepunguza kiwango cha ufadhili kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI;

**Na kwa kuwa**, kwa kulijua hilo serikali ilianzisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) ili kukabiliana na janga hilo;

**Na kwa kuwa**, bado Mfuko huo hauna vyanzo mahususi vya mapato;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuangalia vyanzo hivi ili Mfuko upate fedha za kukabiliana na Janga hili la UKIMWI. Aidha, Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo katika Mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mamlaka ya Umeme Vijijini (*Rural Energy Authority – REA*) ili kusaidia kufanikisha mwitikio huu wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.

Serikali ifikie mahali na kupata ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha hizo. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambapo kwa sasa fedha hizo zimeambatana na masharti magumu. Halikadhalika, kwa mtazamo huu wa Test and Treat inamanisha wigo la wahitaji wa ARVs unazidi kuongezeka wakati wafadhili wanapungua, hivyo hatuna budi kujipanga ili tusije fikia wakati ambapo mahitaji yanazidi uwezo.

3. **Kwa kuwa**, Kamati ilibaini Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kwa asilimia **50**;

**Na kwa kuwa**, hali hii inasababisha:-

a) Tume kushindwa <sup>40</sup> kuajiri watumishi wa

- kutosha kwa baadhi ya Idara na Vitengo na kupelekea nafasi hizo kuendelea kutokujazwa kwa wakati;
- b) Tume kuendelea kuwa na utegemezi wa fedha za nje kwa kutekeleza afua za UKIMWI ambao si endelevu;
  - c) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake hasa katika maeneo ya Ukaguzi wa Ndani, Tathminina Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inayokua kwa kasi duniani; na
  - d) Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania itengewe fedha za kutosha na zipatikane kwa wakati ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

4. **Kwa kuwa**, kumekuwa na upungufu wa dawa aina ya *Septrine* na dawa hizo ni muhimu sana kwa Watu wanaoishi na VVU (WAVIU);

**Na kwa kuwa**, dawa hizi ni muhimu sana kwa kupambana na magonjwa nyemelezi;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri Serikali kwamba, dawa zipatikane kwa wingi nchini lakini pia dawa hizi ziingizwe katika orodha ya dawa (*ARVs package*) ambazo wanapewa WAVIU ili kufubaza makali ya VVU na kuepusha magonjwa nyemelezi.

5. **Kwa kuwa**, kampeni za mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI ni kama<sub>41</sub> zimekufa na hivyo watu sasa

wanafanya ngono zembe bila kuwa na hofu;

**Na kwa kuwa**, ukimya huu husababisha watu kujisahau na hivyo kufanya ngono zembe, hali ambayo inaweza kuleta mfumuko mkubwa hapo baadaye wa maambukizi mapya ya UKIMWI;

**Na kwa kuwa**, tunazo Taasisi ambazo zinatakiwa kufanya kampeni na kuwaelimisha wananchi lakini zimekuwa haziwajibiki ipasavyo;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kuhakikisha Kamati za Udhhibiti wa UKIMWI katika kila ngazi zinafanya kazi ipasavyo. Aidha, Kamati inasisitiza TAMISEMI kuhakikisha vikao vya Kamati za UKIMWI kuanzia ngazi ya Halmashauri, Kata na Mtaa/Vijiji zinawajibika ipasavyo katika mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.

6. **Kwa kuwa**, UKIMWI umeathiri sehemu nyingi za kazi iwe serikalini au katika sekta binafsi;

**Na kwa kuwa**, bila kuwa na mipango thabiti ya kuwalinda watumishi kwa sekta hizi mbili, ukuaji wa uchumi wa Tanzania utashuka na hivyo kuathiri maendeleo ya nchi;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri sekta zote mbili kwa maana ya Serikali na Taasisi zake na Sekta binafsi nchini, iwe ni lazima kutekeleza Mipango ya UKIMWI (HIV/AIDS) mahali pa kazi na taarifa ziwe zikitolewa kwa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI, Tanzania (TACAIDS).

7. **Kwa kuwa**, umri wa maamuzi Tanzania (*Age of Consent*) ni miaka

**Na kwa kuwa**, kuna Mkakati wa UKIMWI wa Kimataifa ujulikanao kama 90, 90, 90; kwa maana ya asilimia 90 ya watu wote wanaokisiwa kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanatambua hali zao za maambukizi, asilimia 90 kati yao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI (ARVs) na asilimia 90 ya hao wanaotumia dawa uwezo wa virusi vyao kuambukiza uwe umefubazwa;

**Na kwa kuwa**, athari za UKIMWI kwa watoto chini ya miaka 18 ni kubwa;

**Na kwa kuwa**, upimaji wa watoto hao hutegemea ridhaa ya wazazi kwa kuwa wao kisheria hawana mamuzi hayo;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri serikali ipunguze umri wa maamuzi binafsi (Age of Consent) kutoka miaka 18 hadi miaka 15 au 16, ili hata Mkakati wa 90, 90, 90, uweze kufanikiwa na kufikia malengo ya tisini – tatu (90 - 3) ifikapo mwaka 2020 na kuumaliza kabisa UKIMWI nchini ifikapo 2030. Aidha, Kamati inashauri suala la upimaji wa VVU lipewe mkazo zaidi ili kuweza kufikia malengo yaliyopo ambapo wigo mkubwa wa WAVIU waweze kujifahamu hali zao na kuanzishiwa dawa ili virusi walivyonavyo viweze kufubazwa na hatimaye kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU miongoni mwa jamii yetu.

8. **Kwa kuwa**, moja ya sababu zinazochangia mabinti wengi kuambukizwa VVU ni ukeketaji wa watoto wetu wa kike (*Female Genital Mutilation - FGM*) kwani wakati mwingine hutumia kifaa

kimoja kukeketa na kwa hivi sasa suala hili hufanyika kwa usiri mkubwa;

**Na kwa kuwa**, jambo hili pia ni kinyume cha haki za binadamu;

**Na kwa kuwa**, baadhi ya waathirika wa jambo hili wanashindwa kutimiza malengo yao kimaisha kutokana na madhara ya ukeketwaji;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri serikali kupiga marufuku ukeketaji na ikiwezekana kuwepo na sheria kuwa ukeketaji hauruhusiwi Tanzania.

9. **Kwa kuwa**, kuna taasisi za kitaifa na za kimataifa zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI nchini;

**Nakwa kuwa**, taasisi hizi hupokea fedha nyingi za UKIMWI;

**Na kwa kuwa**, bado hakuna ufuatiliaji wa kujua fedha hizi zinavyotumika;

**Na kwa kuwa**, Kamati pia ingependa kujua kazi zinazofanywa na taasisi hizo;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kupitia TACAIDS kufuatilia (*coordination*) taasisi hizo zinavyotekeleza kazi zao.

10. **Kwa kuwa**, kukaa bila kazi kunaruhusu makundi ya vijana kujiingiza kwenye vishawishi mbalimbali ikwemo kufanya ngono zembe na hivyo kupata maambukizo ya magonjwa mbalimbali ikiwepo VVU;

**Na Kwa kuwa**, nchi yetu ina fursa ya kilimo kwa maana ya kuwa na ardhi ya kutosha na yenye rutuba;

**Na kwa kuwa**, vijana<sub>44</sub> wakipatiwa rasilimali fedha

wanaweza kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo na kuachana na tabia hatarishi;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mashamba na kuwakopesha vijana mikopo midogo midogo ili waweze kulima mashamba hayo na ikiwezekana wapatiwe mbegu bure mfano za mikorosho ambayo ni kati ya mazao yanayohitajika sana katika soko la dunia hivi sasa.

11. **Kwa kuwa**, yapo makundi maalum ambayo yasipoangaliwa yataleta athari kubwa sana kwa siku za usoni;

**Na kwa kuwa**, makundi yanayofahamika ni watumia madawa ya kulevya (*Injectable Drug Users – IDU*), watu wanaojihusisha na ngono za jinsia moja (*MSM & Lesbians*), watu wanaojiuza (*Sex Workers – SW*);

**Na kwa kuwa**, wanafunzi nao ni kundi hatarishi kutokana na kujihusisha na mahusiano yasiyofaa ya kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja;

**Na kwa kuwa**, hali hiyo ni hatari sana kwa mustakabali wa maisha yao na uchumi wa Taifa;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali iandae Programu Maalum kwa vijana walio ndani na nje ya shule. Ambapo waliopo shuleni waandaliwe klabu maalum zitazohusika na masuala ya VVU na UKIMWI kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Halikadhalika, uanzishwaji wa huduma rafiki kwa vijana (*Youth Friendly Services*) katika kila Mtaa na Kijiji ambazo zitasimamiwa kwa karibu na

kamati za kudhibiti UKIMWI za ngazi ya Mtaa na Kijiji husika.

## xii. SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

#### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2018. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama, Mb na Naibu Waziri Antony Mavunde na Stella Ikupa, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndg. Rogers Siyan'ga na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe



wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb - M/Mwenyekiti
2. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Mary Deo Muro, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Martha Mosses Mlata - Mjumbe
12. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb -Mjumbe
14. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb -Mjumbe
16. Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati<sup>47</sup> za Bunge, Ndg. Athumani

Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

#### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kuikubali na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

.....

Dkt. Jasmin Tiisekwa Bunga, Mb

**MAKAMU MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**

**7 FEBRUARI, 2018**